**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATIKUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

---

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara Morogoro,
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA**

**24 APRILI, 2026**

# YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** .......... i
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... ii
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 1
**1.0 UTANGULIZI** .......... 1
1.1 Muundo wa Taarifa .......... 1
1.2 Msingi wa Uchambuzi .......... 2
1.3 Mawanda ya Uchambuzi .......... 2
**SEHEMU YA PILI** .......... 4
**2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... 4
2.1 Vipengele vya Uchambuzi .......... 4
2.2 Makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026 .......... 5
2.3 Uchambuzi wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti .......... 7
2.3.1 Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria .......... 7
2.3.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali .......... 9
2.3.3 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka .......... 11
2.3.4 Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama .......... 13
2.3.5 Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora .......... 15
2.3.6 Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania .......... 17
2.3.7 Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali .......... 18
2.3.8 Fungu 101 - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria .......... 22
2.4 Tathmini ya jumla kuhusu Mapokezi ya fedha za Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria. .......... 23
2.5 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 .......... 25
2.6 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati .......... 31
**SEHEMU YA TATU** .......... 32
3.**0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** .......... 32
3.1 Maduhuli .......... 32
3.2 Makadirio ya Matumizi katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 .......... 34
3.2.1 Mchanganuo wa Fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027. .......... 34
3.2.2 Mchanganuo wa Fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 .......... 36
**SEHEMU YA NNE** .......... 39
**4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** .......... 39
4.1 Maoni ya Jumla .......... 39
4.2 Ushauri Mahsus Fungu kwa Fungu .......... 39
4.2.1 Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria .......... 39
4.2.2 Fungu 16-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali .......... 40
4.2.3 Fungu 35- Ofisi ya Taifa ya Mashtaka .......... 40
4.2.4 Fungu 55- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora .......... 41
**SEHEMU YA TANO** .......... 43
**5.0 HITIMISHO** .......... 43

# ORODHA YA MAJEDWALI

**JEDWALI NA. 1:** Makusanyo ya Madhuhuli 2025/2026 ........................................... 6

**JEDWALI NA. 2:** Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Februari, 2026 Fungu 41 ..... 8

**JEDWALI NA. 3:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 16 ............. 10

**JEDWALI NA. 4:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026-Fungu 35 ............... 12

**JEDWALI NA. 5:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 12 ............. 14

J**EDWALI NA. 6:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026-Fungu 55 ............... 16

**JEDWALI NA. 7:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 59 ............. 18

**JEDWALI NA. 8:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 19 ............. 20

**JEDWALI NA. 9:** Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 101 ........... 22

**JEDWALI NA. 10:** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026 kwa Wizara na Taasisi zake ....................................................... 24

**JEDWALI NA. 11:** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026 ............... 25

**JEDWALI NA. 12:** Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2026/2027 .............. 35

**JEDWALI NA. 13:** Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2026/2027 ............... 37

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 1.1 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, misingi na muundo wa taarifa hii;

(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/2026 katika

maeneo yanayohusu makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Ofisi hii na Serikali kwa ujumla; na

(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi na Maoni ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na matakwa ya Kanuni ya 121(4) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu 6(2)(e) na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

## 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu nane (8) ambayo ni: -

(a) **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria;

(b) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(c) **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

(d) **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama;

(e) **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(f) **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;

(g) **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; na

(h) **Fungu 101** – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

### 2.1 Vipengele vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao cha Kamati kilichoketi tarehe 10 na 28 Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ikiwa na jumla ya mafungu nane (8) iliyohusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na **Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb)** Waziri wa Wizara hiyo. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: -

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(b) Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.2 Makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 108,332,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria ililenga kukusanya **Shilingi 45,000,000.00**, **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ililenga kukusanya **Shilingi 60,000,000.00** na **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ililenga kukusanya **Shilingi 3,332,000.00**.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hayo hadi kufikia februari, 2026 unaonesha kuwa: -

**(a)** **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria imekusanya zaidi ya lengo la **asilimia 66.7** kwani imekusanya **Shilingi 32,800,000.00** sawa na **asilimia 72.9** ya kiasi kilichoidhinishwa.

Kamati ilielezwa kuwa, Sababu za kuvuka lengo la ukusanyaji maduhuli ni uwepo wa idadi kubwa ya maombi kwa ajili ya usajili na uhuishaji wa vyeti vya Wasuluhishi wa migogoro nje ya utaratibu wa mahakama (*Alternative Dispute Resolution*) na Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria.

**(b)** **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekusanya kiasi cha **Shilingi 56,000,000.00** kati ya **Shilingi 60,000,000.00** sawa na **asilimia 93.33** ya lengo la Makusanyo. Makusanyo hayo yanatokana na wapangaji kuzingatiaji mikataba ya upangishaji wa majengo ya Ofisi hii kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

**(c) Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haikuweza kukusanya kiasi chochote cha fedha, hata hivyo lengo la makusanyo ya ofisi hiyo ni **Shilingi 3,332,000.00** kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati ilielezwa kuwa, Maduhuli hayo yaliyopangwa kukusanywa kutokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Ofisi hiyo kama vile kuuza nyaraka za zabuni, ada mbalimbali na urejeshwaji wa fedha za umma.

Kamati ina maoni kuwa, **ili kufikia lengo lililokusudiwa la makusanyo ya maduhuli, ni ushauri wa Kamati kuwa ni vyema Fungu 16 izingatie uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa kuwianisha na uhalisia wa vyanzo vya makusanyo**.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1 Makusanyo ya Madhuhuli 2025/2026**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO | MAKUSANYO HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 | 32,800,000.00 | 109 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 60,000,000 | 56,000,000 | 93.33 |
| **Fungu 16** – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **108,332,000** | **88,800,000.00** | **81.97** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*.

## 2.3 Uchambuzi wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia bajeti ya Wizara hii, Kamati imeangazia mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida ambayo inajumuisha mishahara (PE) na matumizi mengineyo (OC) pamoja na fedha kwa ajili ya maendeleo. Tathmini ya utekelezaji wa bajeti hadi februari, 2026 kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 97,734,068,000.00**. Katika kiasi hicho, **Shilingi 45,175,295,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikujumuisha **Shilingi 14,182,689,000.00** kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 30,992,606,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Aidha, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ni shilingi **52,558,773,000.00,** ambapo **shilingi 44,415,453,000.00** ni fedha za ndani na **shilingi 8,143,320,000.00** ni fedha za nje.

Hadi kufikia Februari, 2026, Fungu 41 lilikuwa limepokea jumla ya **shilingi 63,405,563,112.50** sawa na **asilimia 64.87** ya kiasi chote kilichoidhinishwa. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo unaonesha kuwa:-

**(a)** Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026 zilizopokelewa **Shilingi 27,361,153,760.61** sawa na **asilimia 61** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha mishahara Shilingi **9,917,208,329.47** sawa na asilimia **69.92,** na matumizi mengineyo **shilingi 17,443,945,431.14** sawa na asilimia **56** ya fedha zilizoidhinishwa.

**(b)** Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia februari, 2026 jumla ya **shilingi 36,044,409,351.89** zimetolewa sawa na **asilimia 68.58** ya fedha zilizoidhinishwa. Kiasi hicho kinajumuisha **shilingi 35,820,179,491.89** fedha za ndani, sawa na **asilimia 80.65** na **shilingi 224,229,860.00** fedha za nje, sawa na **asilimia 2.75**.

Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 2 hapa chini.

**JEDWALI NA. 2: Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Februari, 2026 Fungu 41**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezl |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 30,992,606,000.00 | 17,443,945,431.14 | 56 |
| | Mishahara | 14,182,689,000.00 | 9,917,208,329.47 | 69.92 |
| **Jumla Ndogo** | | **45,175,295,000.00** | **27,361,153,760.61** | **61** |
| Maendeleo | Ndani | 44,415,453,000.00 | 35,820,179,491.89 | 80.65 |
| | Nje | 8,143,320,000.00 | 224,229,860.00 | 2.75 |
| **Jumla Ndogo** | | **52,558,773,000.00** | **36,044,409,351.89** | **68.58** |
| **JUMLA KUU** | | **97,734,068,000.00** | **63,405,563,112.50** | **64.87** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 41 na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini inaonesha kuwa, kiwango cha mapokezi ya fedha za maendeleo kwa upande wa fedha za nje si cha kuridisha, kwani zimepokelewa **asilimia 2.75** tu badala ya **asilimia 66.7**.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani, hali ya mapokezi ilikidhi matakwa ya kibajeti kwani zilipokelewa **asilimia 80.65**. Kamati ilielezwa kuwa, kupokelewa kwa fedha hizo, kumewezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo kutekeleza mradi wa **Mama Samia Legal Aid Campaign**, jambo lililochangia kurudisha tabasamu kwa wananchi waliokuwa wamekosa matumaini na kupunguza chuki dhidi ya Serikali inayosababishwa na baadhi ya watu wanaopoka au kukandamiza haki za watu wanyonge.

### 2.3.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 40,941,954,000.00**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 40,153,250,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ikujumuisha **shilingi 35,481,434,000.00** kwa ajili ya matumizi Mengineyo na shilingi **shilingi 4,671,816,000.00** kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 788,704,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambazo zote ni fedha za ndani kwa ajili

ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa ya Mwanza na Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kuwa:-

**(a)** Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi ilipokea kiasi cha **Shilingi 24,492,796,948.70** sawa na **Asilimia 61** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha Shilingi **21,653,209,016.70** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **2,839,587,932.00** kwa ajili ya Mishahara.

**(b)** Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Februari, 2026, Ofisi ilipokea kiasi cha **Shilingi 179,346,312.00** sawa na **Asilimia 22.74** ya fedha zilizoidhinishwa.

Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 3 hapa chini.

**JEDWALI NA. 3: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 16**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezl |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 35,481,434,000.00 | 21,653,209,016.70 | 61.03 |
| | Mishahara | 4,671,816,000.00 | 2,839,587,932.00 | 60.78 |
| **Jumla Ndogo** | | **40,153,250,000.00** | **24,492,796,948.70** | **61** |
| Maendeleo | Ndani | 788,704,000.00 | 179,346,312.00 | 22.74 |
| **JUMLA KUU** | | **40,941,954,000.00** | **24,672,143,260.70** | **60.26** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 16 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, hali ya mapokezi ya fedha za maendeleo si ya kuridhisha, kwani zilipokelewa **asilimia 22.74** tu badala ya **asilimia 66.7**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kutengwa kwa kiasi kidogo cha fedha kuna hatari ya kuathiri utekelezaji wa ujenzi wa majengo ya Ofisi, hususan jengo la Ofisi la Mkoa wa Arusha kutokukamilika kwa kadiri ilivyopangwa. **Ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati, Kamati inashauri fedha zilizotengwa zitolewe kikamilifu.**

### 2.3.3 Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 145,972,057,000.000.** Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 130,105,947,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ikijumuisha **shilingi 20,343,283,000.00** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 109,671,664,000.00** kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilitengwa kiasi cha **Shilingi 15,866,110,000.00** zote zikiwa ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha hizo inaonesha kuwa:-

**(a)** Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Ofisi ilipokea jumla ya **Shilingi 95,323,562,030.08** sawa na **Asilimia 73.27**

ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 79,663,984,850.00** sawa na **asilimia 72.64** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 15,659,577,180.80** sawa na **asilimia 76.98** ni kwa ajili ya Mishahara.

**(b)** Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Februari 2026, zilipokelewa **shilingi 12,772,517,668.71** sawa na **asilimia 80.5** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo unaonekana katika **jedwali namba 4** hapa chini.

**JEDWALI NA. 4: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026-Fungu 35**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 109,671,664,000.00 | 79,663,984,850.00 | 72.64 |
| | Mishahara | 20,343,283,000.00 | 15,659,577,180.80 | 76.98 |
| **Jumla Ndogo** | | **130,105,947,000.00** | **95,323,562,030.08** | **73.27** |
| Maendeleo | Ndani | 15,866,110,000.00 | 12,772,517,668.71 | 80.5 |
| **JUMLA KUU** | | **145,972,057,000.00** | **108,096,079,698.79** | **74.06** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 35 na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mwaka unaoisha ni ya kuridhisha, kwani katika kila sehemu ya bajeti, zilipokelewa zaidi ya **asilimia 66.7**. Kamati ilielezwa

kuwa, kupokelewa kwa fedha kiasi cha kuridhisha kumesaidia ofisi kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuendesha mashauri ya jinai nchini, ambapo kwa sasa mashauri yote ya jinai ya mahakama za wilaya na mahakama za juu yake zinaendeshwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kutumia watalaam wa sheria. Vilevile kiasi hicho kimewezesha Ofisi ya Mashtaka kufanya ufuatiliaji wa baadhi ya malalamiko yanayohusu masuala ya jinai hususan mashauri yanayoendeshwa katika baadhi ya mahakama za mwanzo ambako Ofisi hiyo haina usimamizi.

Aidha, licha ya mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa bado Ofisi hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo uhaba wa magari na kompyuta. Changamoto hiyo imesababishwa na mahitaji kuwa makubwa kufuatia Ofisi hii kuanzisha Ofisi za Wilaya takribani wilaya zote zilizopo nchini, isipokuwa kwa wilaya ishirini na moja (21).

### 2.3.4 Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume iliidhinishiwa Bajeti ya **shilingi 6,966,967,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo **shilingi 5,841,720,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi

Mengineyo na **shilingi 1,125,247,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026 Tume ya Utumishi wa Mahakama ilipokea jumla ya **shilingi 3,873,051,966.00** sawa na **asilimia 55.59** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Matumizi Mengineyo ni **shillingi 3,317,081,966.00** sawa na **asilimia 56.78** na Mishahara **shilingi 555,970,000.00** sawa na **asilimia 49.41**.

Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika **jedwali namba 5** hapa chini.

**JEDWALI NA. 5: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 12**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 5,841,720,000 | 3,317,081,966 | 56.78 |
| | Mishahara | 1,125,247,000 | 555,970,000 | 49.41 |
| **JUMLA KUU** | | **6,966,967,000** | **3,873,051,966** | **55.59** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria kwa Fungu 12 na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, kiwango cha upokeaji wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida hususan kwa upande wa fedha za matumizi mengineyo kipo chini ya **asilimia 66.7** inayotakiwa,

kwani zilipokelewa kiasi sawa na **asilimia 49.41**. Kupokelewa kwa kiasi kisichofikia lengo kuna hatari ya kuathiri uendeshaji wa shughuli za kila siku za Tume, ikizingatiwa kuwa Tume hii inasamamia watalaam wenye jukumu la kutoa haki nchini ambao ni Majaji na Mahakimu.

### 2.3.5 Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 11,743,965,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,452,519,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 8,291,446,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2026, Tume ilipokea kiasi cha **Shilingi 9,013,978,807.73** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 76.75** ya fedha zilizoidhinishwa ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 2,427,131,000.00** sawa na **asilimia 70.30** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 6,586,847,807.73** sawa na **asilimia 79.44** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

Kwa upande wa fedha za maendeleo, Tume hii haikudhinishiwa kiasi cha fedha. Hata hivyo, ilipokea jumla ya **Shilingi 62,900,125.00** kutoka taasisi ya *Danish Institute for Human Rights* ikiwa ni Mradi wa kuandaa

Mpango kazi wa Haki za Binadamu na Biashara. Fedha hizo zilitumika kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuwezesha mkutano wa kitaifa wa majadiliano na wadau wa biashara katika sekta za kilimo, uzalishaji na usafirishaji kuhusu uimarishaji wa haki za binadamu na uhakiki.

Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 6 hapa chini.

**JEDWALI NA. 6: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026-Fungu 55**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 8,291,446,000.00 | 6,586,847,807.73 | 79.44 |
| | Mishahara | 3,452,519,000.00 | 2,427,131,000.00 | 70.30 |
| **JUMLA KUU** | | **11,743,965,000.00** | **9,013,978,807.73** | **76.75** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizra ya Katiba na Sheria kwa Fungu 55 na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonesha kuwa, mapokezi ya fedha kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa ya kuridhisha. Kupitia fedha hizo, Tume ilitekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kushughulikia na kufunga **malalamiko 76** yaliyohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuwezesha baadhi ya watumishi wa umma kulipwa haki zao ikiwemo haki ya kulipwa fedha za kusafirisha mizigo na madai ya kuumia kazini. Kulipwa huko kunatokana na Tume kufanya uchunguzi na kubaini kuwa watumishi hao wanahaki ya kulipwa na Serikali kutekeleza uamuzi wa Tume, licha ya kwamba mamlaka zao za ajira zilikuwa zimeshafanya uamuzi kuwa watumishi hao hawana haki ya kulipwa.

Aidha, licha ya kazi hizo, Kamati imebaini kuwa Tume hii haina Ofisi kwenye mikoa 26 kati ya mikoa 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kukosekana kwa ofisi hizo kunasababisha Tume kushindwa kupokea na kushughuliki malalamiko ya wananchi wanaoishi katika mikoa isiyokuwa na Ofisi za Tume

### 2.3.6 Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliidhinishiwa na Bunge kutumia kiasi cha **Shilingi 7,402,530,000.00** kwa ajili ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,775,350,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 5,627,180,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2026, Tume ya Kurekebisha Sheria ilipokea kiasi cha **Shilingi 3,894,346,699.61** sawa na **asilimia 53** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi 845,774,199.60** ni Mishahara na **Shilingi 3,048,572,500.01** ni Matumizi Mengineyo. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 7 hapa chini.

**JEDWALI NA. 7: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 59**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa hadi Februari 2026 | Asilimia ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 5,627,180,000.00 | 3,048,572,500.01 | 54 |
| | Mishahara | 1,775,350,000.00 | 845,774,199.60 | 48 |
| **JUMLA KUU** | | **7,402,530,000.00** | **3,894,346,699.61** | **53** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria Fungu 59 na Usanifu wa Kamati*.

### 2.3.7 Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 38,497,754,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 4,779,918,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na kiasi cha

**shilingi 33,717,836,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kwa mwaka unaoisha, Ofisi hii haikupangiwa bajeti ya fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2026 Ofisi imepokea kiasi cha **shilingi 22,758,629,755.29**, sawa na **asilimia 59.12** ya fedha zilizoidhinishwa. Katika kiasi hicho kilichopokelewa, **shilingi 3,216,386,756.00** sawa na **asilimia 67.29** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 19,542,242,999.29** sawa na **asilimia 57.96** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Aidha, mbali na kupokea fedha zilizoidhinishwa, Ofisi pia ilipokea kiasi cha **shilingi 4,774,370,000.00** kwa ajili ya uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya Uchaguzi Mkuu, uliofanyika Oktoba 2025, ambapo Ofisi ilisimamia uendeshaji wa **mashauri 75** ya uchaguzi yaliyofunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 8 hapa chini.

**JEDWALI NA. 8: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 19**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 33,717,836,000 | 19,542,242,999.29 | 57.96 |
| | Mishahara | 4,779,918,000 | 3,216,386,756 | 67.29 |
| **JUMLA KUU** | | **38,497,754,000** | **22,758,629,755.29** | **59.12** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mapokezi ya fedha kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilikuwa ya wastani, kwani zilipokelewa **asilimia 59.12** badala ya **asilimia 66.7**. Licha ya kiasi hicho, Ofisi imetekeleza kazi mbalimbali katika kipindi hicho. Baadhi ya kazi hizo ni kuendesha mashauri ya madai **10,398** yakihusisha madai ya kitaifa **9,585**, madai ya kimataifa **34**, mashauri ya uchaguzi **75** na mashauri ya Kikatiba na Haki za Binadamu **704**.

Katika mashauri **10,398** yaliyosimamiwa na Ofisi hii, katika kipindi cha julai, 2025 hadi februari 2026 yalimalizika mashauri **604** sawa na asilimia **5.81** ya mashauri yote. Katika mashauri 604 yaliyomalizika, Ofisi ilishinda jumla ya mashauri **528** sawa na asilimia **87.42**. Mafanikio yaliyopatikana kupitia ushindi huo ni kuokoa fedha za Serikali kiasi cha **shilingi 295,338,943,322.29**.

Licha ya mafanikio haya, **ni mtazamo wa Kamati kwamba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ibuni mkakati mahsusi utakaowezesha kasi ya umalizaji wa mashauri kuongezeka.** Kumalizika kwa mashauri mapema, kutapelekea wadau husika kufahamu haki zao kwa wakati na hivyo kupunguza malalamiko ya haki kucheleweshwa.

Aidha, pamoja na kazi nyingi zinazotekelezwa na Ofisi hii, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa majengo ya Ofisi kwenye ofisi za Mikoa. Changamoto hiyo imepelekea ofisi kupanga kwenye majengo mbalimbali kwa baadhi ya mikoa, na hivyo kuongeza gharama za matumizi na wakati mwingine kuleta ugumu katika kusimamia mashauri ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii kazi yake kuu ni kusimamia mashauri ya madai yanayoihusu Serikali kwa ujumla ikiwemo mashauri yanayozihusu taasisi, wakala, mashirika ya umma na TAMISEMI bila ya kutoza gharama zozote. **Ili kuondokana na changamoto ya Ofisi kwa baadhi ya mikoa, Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ihakikishe Ofisi hii inapewa vyumba kwa ajili ya ofisi za mikoa hiyo pasipo kulazimu Ofisi hii kulipia kodi ya pango. Aidha, Ofisi ibaki na jukumu la kulipia gharama za uendeshaji wa Ofisi kama vile umeme, maji, usafi na ulinzi**.

### 2.3.8 Fungu 101 - Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**; Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 17,382,964,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,454,158,000.00** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 928,806,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Hadi kufikia Februari 2026, Ofisi imepokea kiasi cha **Shilingi 11,240,807,766.67** sawa na **Asilimia 65** ya bajeti iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 10,183,150,766.67** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 1,057,657,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Mchanganuo wa bajeti iliyoidhinishwa unaonekana katika jedwali namba 9 hapa chini.

**JEDWALI NA. 9: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 - Fungu 101**

| Fedha | Matumizi | Fedha Ilioidhinishwa | Fedha Iliyopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | OC | 16,454,158,000 | 10,183,150,766.67 | 61.89 |
| | PE | 928,806,000 | 1,057,657,000.00 | 113.88 |
| **JUMLA KUU** | | **17,382,964,000** | **11,240,807,766.67** | **65** |

***Chanzo:*** *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*.

**Mheshimiwa Spika**; Kwa kuwa kazi ya kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili imekamilika, Kamati inapendekeza sheria hizo zitangazwe rasmi na kusambazwa kwa watumiaji ili jamii iweze kuanza kunufaika nazo kama ilivyokusudiwa

## 2.4 Tathmini ya jumla kuhusu Mapokezi ya fedha za Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba: -

(a) Kwa ujumla, Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2025/2026, hadi kufikia Februari, 2026 ilipokea **asilimia 66.56** ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kipindi ambacho ilitakiwa kuwa **asilimia 75** ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa maana hiyo, mtiririko wa upatikanaji wa fedha ulipaswa kuboreshwa zaidi.

(b) Taasisi Mbili (2) kati ya Taasisi Nane (8) zilizopo chini ya Ofisi hii zimefanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 10** na **Jedwali Na. 11.**

**JEDWALI NA. 10: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026 kwa Wizara na Taasisi zake**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2025/2026 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 45,175,295,000.00 | 27,361,153,760.61 | 61 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 40,153,250,000.00 | 24,492,796,948.70 | 61 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 130,105,947,000.00 | 95,323,562,030.08 | 73.27 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 6,966,967,000.00 | 3,873,051,966.00 | 55.59 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 11,743,965,000.00 | 9,013,978,807.73 | 76.75 |
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 7,402,530,000.00 | 3,894,346,699.61 | 53 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 38,497,754,000.00 | 22,758,629,755.29 | 59.12 |
| **FUNGU 101** – Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | 17,382,964,000.00 | 11,240,807,766.67 | 65 |
| **JUMLA KUU** | **297,428,672,000.00** | **197,958,327,734.69** | **66.56** |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 11: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2025/2026 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 52,558,773,000.00 | 36,044,409,351.89 | 68.58 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 788,704,000.00 | 179,346,312.00 | 22.74 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 15,866,110,000.00 | 12,772,517,668.71 | 80.5 |
| **JUMLA KUU** | **69,213,587,000.00** | **48,996,273,332.60** | **70.79** |

***Chanzo**: Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

## 2.5 Ukaguzi wa Miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 inaweka masharti kwa Kamati za kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha (2025/2026) kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Katika kuzingatia masharti hayo, Kamati ilikagua miradi miwili (2) iliyopo katika mkao wa Singida na Mwanza inayotekelezwa na Wizara hii. Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

### (i) Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Singida (Mradi Na 6389)

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 Machi, 2026 Kamati ilitembelea na kukagua ujenzi wa jengo la ghorofa moja kwa ajili ya Ofisi ya Mashtaka Mkoa wa Singida. Ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 10 Machi, 2025 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 10 Machi, 2026. Jumla ya gharama za ujenzi wa mradi huo ni **shilingi 2,402,417,178.00** ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua mradi huu tarehe 12 Machi, 2026, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 38.2,** na malipo ya kiasi cha **shilingi 779,429,999.9** yalikuwa yamefanyika sawa na **asilimia 32** ya gharama zote za mradi. Gharama hizo zinajumuisha ujenzi wa boma, kibanda cha mlinzi, uzio, jengo kwa ajili ya jenereta na uwekaji wa umeme. Ilielezwa kuwa, gharama za mifumo ya TEHAMA pamoja na samani za ofisi si sehemu ya mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mradi huu kutakiwa kukamilika tarehe 30 Machi, 2026, utekelezaji wake haukukamilika katika muda huo na sasa unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2026 baada ya kutolewa muda wa nyongeza wa miezi mitatu. Kamati ilielezwa kuwa, sababu kuu za mradi kutokukamilika kwa wakati ni

kuchelewa kupata fedha za utekelezaji kutoka hazina. Ilielezwa kuwa, licha ya Mkataba kusainiwa tarehe **10 Machi, 2025**, fedha za malipo ya awali (advance payment) zilitolewa mwezi **Julai, 2025** na Mkandarasi alilipwa fedha hizo **mwezi Septemba, 2025**, na hivyo kupelekea mradi kuchelewa kuanza kwa muda miezi sita.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, muda halisia uliotumika kutekeleza mradi huu ni miezi minne, kwani ujenzi ulianza mwezi Septemba, 2025 badala ya mwezi Machi, 2025. Ujenzi kufikia **asilimia 38.2** katika kipindi cha miezi minne tu, ni hatua kubwa na nzuri ya utekelezaji wa mradi huu. **Ili kumuwezesha Mkandarasi kuendelea na kasi nzuri ya utekelezaji wa mradi huu, Kamati inashauri Serikali ihakikishe inatoa fedha za mradi huu kwa wakati**.

**(ii) Ujenzi wa Jengo la Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria - Buswelu, Ilemela- Mwanza (Namba ya Mradi 6389)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa Ofisi wa jengo la ghorofa tatu kwa ajili ya Ofisi za taasisi za kisheria za Serikali katika mkoa wa Mwanza. Taasisi hizo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Kabidhi wasii (RITA).

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 26 Aprili, 2022 na ulitakiwa kukamilika tarehe 25 Oktoba, 2023. Gharama za utekelezaji wa mradi ni jumla ya **shilingi 3,368,671,233.81**, ambapo **shilingi 3,283,227,983.81** ni gharama za mkandarasi SUMA JKT anayetekeleza mradi huu, na **shilingi 85,443,250.00** ni kwa ajili ya Wakala wa Majengo (TBA) kwa ajili ya ushauri elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe **16 Machi, 2026**, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 74**. Aidha, jumla ya kiasi cha **shilingi 2,942,687,466.81** sawa na **asilimia 87.35** ya gharama za mradi zilikuwa zimelipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Katika kiasi hicho, SUMA JKT ilikuwa imelipwa **shilingi 2,887,149,354.81** sawa na **asilimia 88** ya gharama za mkataba wa ujenzi, na TBA ilikuwa imeshalipwa **shilingi 55,538,112.00** sawa na **asilimia 65** ya gharama za Mkataba wa ushauri elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** awali ujenzi wa mradi huo ulitakiwa kukamilika tarehe 25 Oktoba, 2023. Kutokana na kutokumalizika kwake, Serikali imekuwa ikiongeza muda kwa nyakati tofauti tofauti, ambapo nyongeza ya muda iliyotolewa kwa sasa inamalizika tarehe 30 Mei, 2026.

Kuhusu sababu za kutokukamilka kwa mradi huo licha ya kuchelewa kwa muda wa miezi ishirini na tisa (29), Kamati ilielezwa kuwa kuchelewa huko kulisababishwa na uwepo wa mawe kwenye ardhi yaliyogundulika wakati wa uchimbaji wa msingi, na hivyo kusababisha ujenzi wa msingi kuchukua muda mrefu. Aidha, sababu nyingine iliyoelezwa ni ucheleweshaji wa malipo ya fedha kutoka Wizara ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa uwepo wa mawe katika eneo hilo si sababu ya kuchelewa kwa mradi kama ilivyo elezwa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, Kamati hii ilipotembelea na kukagua mradi huu huu mwezi Machi, 2023 wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi, ilielezwa kuwa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 45** ambapo msingi na boma vilikuwa tayari vimeshajengwa. Hivyo basi, kazi ya ujenzi wa msingi ilikamilika tangu mwaka 2023, na hivyo uwepo wa mawe si sababu iliyosababisha mradi huo usikamilike kwa kipindi cha kuanzia mwezi Machi, 2023 hadi Kamati ilipotembelea na kukagua tena mradi huu tarehe 16 Machi, 2026.

Aidha, kuhusu sababu ya kuchelewa kwa malipo kutoka Wizara ya fedha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa nayo si sababu ya kutokukamilika kwa

ujenzi wa jengo hilo katika muda wa nyongeza wa zaidi ya miezi ishirini na tisa. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba, wakati Kamati ilipokagua mradi huu, malipo yaliyokuwa yamelipwa na Serikali kwa mkandarasi SUMA JKT yalikuwa ni **asilimia 88**, wakati kazi ilikuwa imefikia **asilimia 74**. Aidha, Kamati ilipohoji zaidi kuhusu mtiririko wa malipo ya fedha, Mkandarasi hakuwa na jawabu juu ya jambo hilo, na kukiri kuwa tayari alishalipwa **asilimia 88** ya gharama ya Mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati ilipokagua mradi huo mwezi Machi, 2023 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 45**, na ilipoukagua tena mradi huo mwezi Machi, 2026 utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 74**, sawa na utekelezaji wa **asilimia 29** kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu. Kwa mchanganuo huo, mkandarasi huyo anatekeleza mradi huo kwa kiwango cha **asilimia 9** kwa mwaka. Ikiwa hali itaendelea kuwa hivyo, mkandarasi mjenzi atahitaji kutumia muda wa miaka miwili na miezi nane kumaliza ujenzi uliobakia ambao ni sawa na **asilimia 26**.

**Mheshimiwa Spika,** katika mazingira hayo, tathmini inaonesha kuwa hali halisi ya utekelezaji wa mradi huu unaojengwa na SUMA JKT si ya kuridhisha. Aidha, kwa kuwa mkandarasi huyo alishalipwa kiasi kikubwa cha fedha kwa kinachozidi kazi aliyotekeleza, na kwa kuwa

hakuna sababu nyingine iliyopo ya mkandarasi kuchelewesha mradi huo, ni mtazamo wa Kamati kuwa kazi hiyo imechelewa kutokana na aidha kwa sababu za uzembe wa Mkandarasi au kwa sababu mkandarasi hana uwezo wa kutekeleza kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo na ili kuunusuru mradi huo, **ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka za kuhakikisha mradi huo unakamilika, na kama ikibidi kumnyang`anya mkandarasi kazi hiyo na kupewa mkandasi mwingine mwenye uwezo**.

## 2.6 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, mnamo tarehe 28 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi. Tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 105,000,000.00** kutoka katika mafungu mawili ambayo ni Fungu 41-Wizara ya Katiba na Sheria jumla ya **shilingi 45,000,000.00** na Fungu 35-Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kiasi cha **shilingi 60,000,000.00**. Vyanzo vya maduhuli hayo ni malipo ya pango kwa kukodisha kumbi, makato kwa watumishi watakaoshindwa kurejesha taarifa ya matumizi ya fedha za masurufu yaliyopewa, ada za watoa huduma wa msaada wa kisheria na watatuzi wa migogoro kwa njia mbadala.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ulinganisho kati ya makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 na 2026/2027, maduhuli yam waka ujao yamepungua kwa kiasi cha **shilingi 3,332,000.00** ikilinganishwa na mwaka unaoisha, ambao maduhuli yalikuwa **Shilingi 108,332,000.00**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kupungua kwa kiasi hicho kunatokana na Fungu 16-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutokuwa na bajeti ya makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2026/2027, ilhali mwaka unaoisha Ofisi hiyo ilikuwa na makadirio ya maduhuli **shilingi 3,332,000.00.**

Wakati Kamati ilipokutana Serikali, ilielezwa kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikiweka bajeti ya makadirio ya maduhuli ikitegemea chanzo kikuu ambacho ni makato ya fedha kwa watumishi watakoshindwa kuwasilisha taarifa ya matumizi ya fedha za masurufu walizopewa, chanzo ambacho kwa sasa hakifanyi kazi kutokana na Serikali kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Aidha, kwa upande wa Fungu 35 na Fungu 41, makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yamebaki kama yalivyokuwa katika mwaka wa fedha 2025/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya Mafungu manane (8) yaliyopo chini ya Wizara hii, ni Mafungu Mawili pekee ndiyo yenye Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Hali hiyo inatokana na asili na majukumu ya kila Fungu, ambapo

mafungu mengi yamejikita katika kutoa huduma isiyokuwa na tozo, ada, na adhabu .

## 3.2 Makadirio ya Matumizi katika Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Katiba na Sheria katika mafungu yake nane inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 487,166,693,000.00**. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 372,427,763,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha **shilingi 57,156,323,000.00** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 315,271,440,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, kiasi cha **shilingi 114,738,930,000.00** kinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ulinganisho kati ya bajeti ya Mwaka 2025/2026 na bajeti ya mwaka 2026/2027, bajeti ya mwaka unaofuata imeongezeka kwa kiasi cha **shilingi 118,524,387,000.00** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa ni **shilingi 368,642,306,000.00**. Ongezeko hilo ni wastani wa **asilimia 32.15**.

### 3.2.1 Mchanganuo wa Fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Aidha, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, bajeti yam waka 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha

**shilingi 74,999,091,000.00,** sawa na **asilimia 22.22**, ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya mwaka wa Fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa ni **shilingi 297,428,672,000.00.** Katika kiasi hicho, mishahara imeongezeka kwa **shilingi 5,805,695,000.00** sawa na **asilimia 11.3** ikilinganishwa na mwaka unaoisha, na fedha za matumizi ya mengineyo (OC) zimeongezeka kwa kiasi cha **shilingi 72,193,350,000.00** sawa na **asilimia 29.7** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026.

Mchanganuo wa bajeti ya Kawaida umeainishwa katika **jedwali Na12**

**JEDWALI NA. 12: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2026/2027**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 15,721,630,000.00 | 49,738,345,000.00 | 65,459,975,000.00 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,809,900,000.00 | 52,281,434,000.00 | 57,091,334,000.00 |
| **Fungu 35** - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 22,251,348,000.00 | 124,405,864,000.00 | 146,657,212,000.00 |
| **Fungu 12** - Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,1017,424,000.00 | 7,130,120,000.00 | 8,147,544,000.00 |
| **Fungu 55** - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 4,115,311,000.00 | 13,291,446,000.00 | 17,406,757,000.00 |

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 59** - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania | 1,556,429,000.00 | 10,555,230,000.00 | 12,111,659,000.00 |
| **Fungu 19** - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 5,095,940,000.00 | 36,217,836,000.00 | 41,313,776,000.00 |
| **Fungu 101 –** Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria | 2,588,341,000.00 | 21,651,165,000.00 | 24,239,506,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **57,156,323,000** | **315,271,440,000.00** | **372,427,763,000.00** |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

### 3.2.2 Mchanganuo wa Fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo, bajeti ya mwaka 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi **43,525,296,000.00** sawa na **asilimia 61.12** ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa shilingi **71,213,634,000.00.**

Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 13**

**JEDWALI NA. 13: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2026/2027**

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | |
|---|---|---|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 41** - Wizara ya Katiba na Sheria | 94,425,953,000.00 | 446,867,000.00 |
| **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,000,000,000.00 | - |
| **FUNGU 35 –** Ofisi ya Taifa ya Mashitaka | 15,866,110,000.00 | - |
| **JUMLA NDOGO** | **114,292,063,000.00** | **446,867,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **114,738,930,000.00** | |

***Chanzo***: *Randama za Wizara ya Katiba na Sheria na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya ujumla inaonesha kuwa bajeti yam waka 2026/2027 imeionggezeka katika kila kipengele, isipokuwa tu kwa fedha za maendeleo za nje. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

Kwa upande wa matumizi ya kawaida, Kamati ilielezwa kuwa, ongezeko katika matumizi ya kawaida linatokana na mabadiliko ya muundo wa utumishi na mishahara yaliyofanyika kwa baadhi ya taasisi ambpo mabadiliko

hayo yataanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaofuata.

Aidha, baadhi ya taasisi ziliongezewa fedha ili ziweze kuongeza kasi ya kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kuendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050. Baadhi ya taasisi hizo ni Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo inajukumu la kuchambua na kurekebisha sheria ili ziendane na matakwa ya Dira hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, fedha za maendeleo zimeongezeka kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi na kutekeleza mradi wa *Mama Samia Legal Aid Campaign*. Aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**,** ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

(a) Taasisi nyingi chini ya Wizara hii zinakumbwa na changamoto ya majengo ya ofisi, hususan ofisi za mikoa. Aidha, kwa asilimia kubwa bajeti ya fedha za maendeleo inayohusu ujenzi wa ofisi hizo haikutolewa kikamilifu. Ili kutatua changamoto hiyo na kufikisha huduma kwa wananchi, Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kikamilifu.

### 4.2 Ushauri Mahsus Fungu kwa Fungu

#### 4.2.1 Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

(a) Kwa kuwa mradi wa msaada wa huduma za kisheria unaojulikana kama *Mama Samia Legal Aid Campaign*

umekuwa na manufaa kwa wananchi hasa wa hali ya chini kwa kuwapatia haki zao na hivyo kupunguza malalamiko, ili mradi huo uendelee kuleta tabasamu na matumaini kwa watu hao, Serikali iuendeleze mradi huo kwa kuwafikia wananchi mbalimbali hususan wananchi wa vijijini na maeneo mengine ya kimkakati yanayolalamikiwa kukithiri kwa migogoro mbalimbali.

### 4.2.2 Fungu 16-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mshitiri wa ujenzi wa kituo jumuishi cha kisheria katika mkoa wa Mwanza kilichoanza ujenzi mwaka 2022 na kutakiwa kukamilika mwaka 2023. Aidha, Kamati ilipofanya ukaguzi wa mradi huo tarehe 18 Machi, 2026 ilikuta utekelezaji wake umefikia **asilimia 74** licha ya Serikali kufanya malipo kwa kiasi cha **asilimia 88**, ili kuhakikisha mradi huo unakamilika licha ya kuchelewa kwa zaidi ya **miezi 29**, Serikali ihakikishe inachukua hatua za haraka ili kuhakikisha SUMA JKT anakamilisha mradi huo licha ya mtindo wa utekelezaji wake unaosuasua.

### 4.2.3 Fungu 35- Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

(a) Ofisi ya Mashtaka imefanikiwa kuchukua jukumu la kusimamia na kuendesha mashauri ya jinai kote nchini kwa mashauri yanayofunguliwa mahakama za wilaya, mikoa, mahakama kuu na rufaa za mahakama ya

rufani. Uwezekano huu umechangiwa na Ofisi hii kuanzisha Ofisi za mashtaka katika wilaya mbalimbali, isipokuwa kwa wilaya ishirini na moja tu (21). Kutokuwepo kwa Ofisi katika wilaya hizo 21 kuna athiri utekelezaji wa jukumu la kushtaki na kusimamia mashauri ya jinai katika wilaya hizo. Ili kuondokana na changamoto hiyo, Serikali ianzishe ofisi za mashtaka katika wilaya zilizobakia.

(b) Katika wilaya ambazo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzisha ofisi za mashataka za wilaya na kuteuwa wakuu wa mashtaka wa wilaya, kuna changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi muhimu ikiwemo magari na kopyuta, na hivyo kusababisha mazingira ya kufanya kazi katika wilaya hizo kuwa magumu. Ili watendaji waliopo katika ofisi hizo waweze kufanya kazi kwa ufanisi, Kamati inashauri kuwa Serikali inunue vitendea kazi muhimu ikiwemo magari, kompyuta na mashine za kudurufu.

### 4.2.4 Fungu 55- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

(a) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora, na kufanikisha watu mbalimbali kupata haki zao. Licha ya mafanikio haya, Tume hii

ina Ofisi katika mikoa mitano (5) tu kati ya mikoa 31 iliyopo nchini. Kukosekana kwa ofisi hizo, kumekuwa na athari za Tume kushindwa kufikiwa na wananchi wengi wa mikoa iliyobakia ili waweze kusaidiwa katika kupata haki zao. Ili kuondokana na changamoto hii, Serikali iiwezeshe Tume ili iweze kuanzisha Ofisi katika mikoa 26 iliyobakia.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - **Mjumbe**
4. Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - **Mjumbe**
5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - **Mjumbe**
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - **Mjumbe**
7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb - **Mjumbe**
8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb - **Mjumbe**
9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb - **Mjumbe**
10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb - **Mjumbe**
11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb - **Mjumbe**
12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb - **Mjumbe**
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - **Mjumbe**
14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb - **Mjumbe**

15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb - **Mjumbe**
16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb - **Mjumbe**
17. Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb - **Mjumbe**
18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb - **Mjumbe**
19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb - **Mjumbe**
20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb - **Mjumbe**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, **Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb)**) –Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na Mhe. Zainabu Athuman Katiba (Mb)-Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wameendelela kuipatia Kamati yetu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Eliakim Chacha Maswi na Naibu Katibu Mkuu wake Dkt. Franklin Jasson Rwezimula.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

24 Aprili, 2026